TANGAZO LA SERIKALI Na. 218 la tarehe 24/3/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI,
(SURA YA 355)

---

**AMRI**

---

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

---

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA MSASA YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itaitwa Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Eneo la Msasa ya Mwaka 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (Mpango wa Urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina katika eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

“Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba A yenye majira - nukta 339268MS, 9628626KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini- Magharibi katika uelekeo wa $121^0$ kwa umbali wa kilomita 0.3 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba B yenye majira - nukta 339140MS, 9628944KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kasini – Magharibi katika uelekeo wa $135^0$ kwa umbali wa kilomita 0.3 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba C yenye majira - nukta 338821MS, 9629075KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskusini - Magharibi katika uelekeo wa $116^0$ kwa umbali wa kilomita 0.4 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba D yenye majira - nukta 338595MS, 962886KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini- Magharibi katika uelekeo wa $81^0$ kwa umbali wa kilomita 0.06 kupitia Runzewe hadi barabara kuu ya Ushirombo hadi alama ya mpaka ya upimaji namba E yenye
majira - nukta 338573MS, 9628809KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi katika uelekeo wa $67^0$ kwa umbali wa kilomita 0.1 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba F yenye majira - nukta 338528MS, 962866KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Mashariki katika uelekeo wa $122^0$ kwa umbali wa kilomita 0.2 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba yenye majira ya nukta 338706MS, 9628455KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa $173^0$ kwa umbali wa kilomita 0.3 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba H yenye majira – nukta 338916MS, 9628267KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Mashariki katika uelekeo wa $98^0$ kwa umbali wa kilomita 0.2 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba I yenye majira - nukta 339081MS, 9628404KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Mashariki katika uelekeo wa $78^0$ kwa umbali wa kilomita 0.06 kupitia Runzewe hadi ulipoanzia’’

Dodoma,
6 Februari, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*